# KARISMATIKI KATOLIKI ILIVYOANZA

## Taarifa ya mwenye kushuhudia kwa macho yake

**Imeandikwa**
**na**
**Patti Gallagher Mansfield**

**Imetafsiriwa na Padri Theo Van Schayk**

**Kipigo chapa cha Mtandao**
**2020**

**Agape Publications**
**P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam**
**Simu : + 255 767 342068**
e-mail : kungwecentre@gmail.com
kungwecentre@outlook.com

# Dibaji

**Karismatiki** ni mkondo wa namna gani, na imeanzaje ? Ni nani aliyeanzisha ?

Katika kurasa zifuatazo Mama Patti Gallagher Mansfield, ambaye ni kiongozi katika Karismatiki anayejulikana katika nchi mbalimbali na ni mama wa watoto wanne, anatupatia majibu ya msingi anapoeleza kwa njia inayogusa moyo ile asili ya Mungu kujitia kati, yaani tendo lile la enzi la Mungu lililo shina la Karismatiki Katoliki iliyopo duniani kote siku hizi. Anajua anaongea juu ya nini, kwa sababu alikuwa shahidi wa kwanza wa tukio lote lile.
Wakarismatiki hawana budi kufahamu vizuri mwanzo wa mkondo ambao wanakiri kwamba wamo. Lakini pia wale ambao hawamo, kwanza kabisa maaskofu, halafu mapadre, watawa na makatekista, watapata katika kurasa zinazofuata ufunguo wa kufahamu kazi ya ndani ya mkondo huo.

Kwa maana hatua za kiroho zinazoelezwa na Patti, yaani :

Njaa ya kumfahamu Mungu binafsi
Toba/kuwa tayari kujitenga na dhambi
Kutoa maisha yake kwa mapenzi ya Mungu
Mang'amuzi ya upendo wa Mungu (ambayo ni sawa na mang'amuzi ya Roho Mtakatifu)
Kugundua vipaji vya pekee kwa ajili ya huduma katika Kanisa (Karama)
Kugundua utume wa kumpeleka Yesu ulimwenguni (Uinjilishaji)

Zinabaki kuwa muhimu sana siyo tu kwa maisha ya kila siku ya Wakarismatiki katika Afrika, bali pia kwa mkondo wowote wa kiroho ulio halisi katika Kanisa.

Msomaji mpendwa, upate katika kurasa zifuatazo siyo tu mwanga ili kufahamu kiakili Karismatiki, bali pia upate msukumo kwa maisha ya kiroho yaliyo ya ndani zaidi ambayo yatazidi kuzaa matunda katika huduma ya taifa la Mungu katika Kanisa.

Padri Ernst Sievers, M.afr.
Mratibu wa Karismatiki, Uganda.

# Karismatiki Katoliki ilivyoanza Taarifa ya mwenye kushuhudia kwa macho yake.

Napenda kuanza kwa kushirikisha fungu la kwanza la Maandiko Matakatifu Bwana alilonipa. Saa chache baada ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu, nilijisikia naongozwa kufungua Biblia yangu popote pale nikayaona maneno hayo. Kila mara nilipokuwa na nafasi ya kuongea juu ya yale yaliyotukia huko Duquesne, nimeanza na maneno hayo toka Luka, na ni maneno yaliyotoka katika mdomo wa Maria, Mama yetu.

> "Moyo wangu wamwadhimisha Bwana,
> na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu ;
> kwa kuwa ameutazama
> unyonge wa mjakazi wake.
> Kwa maana, tazama, tokea sasa
> Vizazi vyote wataniita mbarikiwa;
> Kwa kuwa mwenye nguvu amenitendea makuu,
> Na jina lake ni takatifu.
> Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi
> Kwa hao wanaomcha." Lk 1:46-50.

Leo jioni naweza kusema kwamba Mungu aliye na Nguvu amenifanyia mimi makuu – wala siyo tu kwangu mimi binafsi, bali kwetu sisi sote. Jina lake ni Takatifu! Na huruma yake, huruma ambayo imegusa maisha ya

kila mmoja wetu kwa ndani sana, hudumu kwelikweli kizazi hata kizazi kwa wale wanaomcha.

Nianze kidogo na matukio yaliyotukia kabla ya siku ile nilipopokea fungu la Maandiko Matakatifu nililotaja hapo juu, na kukusimulia kuhusu matukio yaliyoelekea kwenye wikiendi ya Duquesne. Nililelewa huko New Jersey (Marekani) katika familia nzuri ya kikatoliki. Siku zote nilitamani kuwa mwema na kujua zaidi kuhusu Mungu, lakini nilijisikia kana kwamba sikujua kwa kutosha juu ya imani ya kikatoliki kwa vile sikuwa na nafasi kamwe kusoma katika shule ya kikatoliki. Rafiki zangu wengi walikuwa Wayahudi.

Nilipotaka kujiandikisha katika Chuo Kikuu, nilitafuta Chuo Kikuu kizuri cha kikatoliki ambapo ningeweza kujifunza Kifaransa na idadi ya wanaume na wanawake ilingane (kwa sababu nilitumaini kuolewa na fulani pale), lakini hasa nilitafuta mahali ambapo ningeweza kujifunza mengi zaidi kuhusu imani yangu na kukutana na wanaume na wanawake wengine wakatoliki. Kwa njia ya kufuta ile na ile, nilifika kwenye Chuo Kikuu cha Duqesne, ambacho jina lake kamili ni Chuo Kikuu cha Roho Mtakatifu cha Duquesne. Kwa kweli maneno juu ya alama ya Duquesne ni haya : « **Ni Roho Mtakatifu anayetoa uhai** ». Yanahusika sana !

Nikaanza mwaka wangu wa kwanza huko Duquesne nikichukua Teolojia 101. Nikaona kwamba ingawa ilifaa kuchukua kozi hii ya teolojia, haikuwa nilichotafuta hata kidogo. Muhula ya pili ya mwaka nilichukua kozi nyingine, halafu mwaka uliofuata nikasoma teolojia

zaidi. Polepole nikaanza kugundua kwamba nilichotafuta kweli, yaani **ambacho nilikuwa na njaa nacho**, hakikuwa tu kujua zaidi juu ya Mungu, bali **kumjua Mungu** – kumfahamu kwa njia ya ndani zaidi – kumfahamu kwa njia ya binafsi.

Nilikuwa na rafiki aliyehudhuria Misa kila siku. Msichana huyo alikuwamo katika kikundi kinachojifunza Maandiko Matakatifu katika campus inayoitwa Chi Rho. Walikutana mara moja kwa wiki ili kujifunza Maandiko Matakatifu na kusali pamoja. Rafiki huyo alinialika nifike katika mkutano mmojawapo. Kwa kweli, alinifuata mwaka mzima nijiunge na Mafundisho hayo ya Maandiko Matakatifu. Na mimi nilitoa kila aina za sababu za kubuni, kwa nini siwezi kwenda. Kimsingi nilikwama. Nilivutwa kumjua Mungu zaidi, lakini niliogopa. Niliogopa atakayotaka kwangu. Niliogopa kwamba mipango yake juu ya maisha yangu yanaweza kupingana na mipango yangu juu ya maisha yangu, na mipango yangu ni mingi. Lakini baada ya mwaka mmoja hatimaye nilikutana na vijana wengine katika kikundi. Nikavutiwa na urafiki wao na wema na ukarimu wao. Na hivi nikaamua kwamba nitakaporudi Duquesne kama mwanfunzi wa mwaka wa pili, nitajiunga nao mara moja kwa wiki kujifunza Maandiko Matakatifu. Na ndivyo nilivyofanya.

Baada ya miezi michache tuliambiwa kwamba kikundi kitafanya ritriti yake ya mwaka. Uamini usiamini, sijawahi kuwa katika ritriti maisha yangu yote. Basi, mara nyingine tena nikawa na maelekeo yanayopingana. Nilivutwa kwenda, kwa sababu nilijua itakuwa

mang'amuzi ya Mungu na wakati huohuo niliogopa. Kwanza tuliambiwa kwamba mada ya ritriti itakuwa Hotuba mlimani. Kwa bahati nzuri haikuwa mada iliyochaguliwa baadaye. Tungalijifunza maneno yote Yesu aliyosema katika hotuba hiyo, tunaglikuwa bado tunakosa nguvu ya kutekeleza amri zake. Halafu tulisikia kwamba lengo la ritriti litakuwa Nafsi na kazi ya Roho Mtakatifu. Ili kujitayarisha kwa ritriti tuliambiwa kusoma sura nne za kwanza za Matendo ya Mtime na kitabu kidogo kinachoitwa "*The cross and the swtichblade*" (Msalaba na bapa la kisu).

Niliposoma "*The cross and the switchblade*" (kwa wale ambao hawajui kitabu hicho, ni masimulizi ya mchungaji wa kipentekoste, David Wilkerson, aliyeongozwa na Roho Mtakatifu kwenda katika jiji la New York kufanya kazi yake ya kichungaji kati ya waliokuwa sugu sana wa dawa ya kulevya), sikuona habari zozote juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuongea katika lugha. Kilichonigusa kweli kilikuwa kwamba kulikuwa na mtu hapa ambaye anaishi katika wakati wetu na ambaye anajua mapenzi ya Mungu. Mungu anaongea naye kwa njia mbalimbali na anamwongoza. Nilisikia hamu ya kuongozwa na Bwana inapanda katika moyo wangu. Niliendelea kufikiri jinsi ambavyo ingekuwa vizuri na ya ajabu, ikiwa mtu wa kawaida kama mimi mwenyewe ningeweza kweli kufahamu uongozi wa Mungu katika maisha yangu. Lakini niliona kwamba aina hii ya uongozi ipo tu kwa ajili ya watu wa pekee kama mapadre, masista na wahudumu wengine. Hakika mwanafunzi wa kawaida kama mimi, basi, hawezi kugundua mapenzi ya Mungu hivi. Hata hivyo nilikuwa

na imani ya kutosha moyoni mwangu hata nikaweza kupiga magoti mbele ya kitanda changu baada ya kumaliza kitabu kile na nikiwa peke yangu katika chumba cha kulala nilisali sala hii: “Bwana, ninaamini kwamba nimekwisha mpokea Roho Mtakatifu wako katika Ubatizo na Kipaimara, lakini kama Roho wako Mtakatifu anaweza kutenda zaidi katika maisha yangu kuliko alivyofanya mpaka sasa, basi, naomba iwe hivyo!” Na baada ya kusali sala hiyo, nilifungua macho yangu nakatazama huko na huko katika chumba changu. Sijui nilichotegemea kuona – maono, malaika, kitu cha ajabu. Sikuona chochote, hakika sikujisikia tofauti kabisa na nilijiambia mwenyewe: “Kamwe sitamwambia mtu yeyote kwamba nilisali sala hiyo”. Basi, mniamini kwamba  ninyi si watu wa kwanza niliowaambia kuhusu sala hiyo! Nilifikiri kwamba kwa sababu sikuona chochote cha ajabau wakati ule, Mungu hakusikia sala yangu. Je, unajua niliombea nini ? Niliombea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sikutumia maneno yatumikayo kwa kumwomba Roho Mtakatifu aje, lakini njaa yangu ndiyo ilikuwa ya kumpokea Roho Mtakatifu.

Siku chache baadaye wanafunzi kama 25 au 30 waliondoka kwenda kwenye ritriti. Jioni ile ya kwanza tulipata mafundisho juu ya Maria. Yalifundishwa na mmoja wa maprofesa ambaye nilimjua kwa vile ni mwalimu wangu wa teolojia. Alipoongea juu ya Maria kama mwanamke wa imani na mwanamke wa sala, nilimwona kwamba ni mtu mwingine, si kama nilivyomzoea. Nikawaza : « Anaonekana na utulivu, amani na heri sana – karibu kana kwamba amejazwa na Roho Mtakatifu ». Kitu ambacho sikujua kilikuwa

kwamba profesa huyo, mke wake na maprofesa wengine wawili wa Duquesne walipata bahati ya kusoma vitabu vichache juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Walisoma « *the cross and the switchblade* » na walisoma kitabu kinachoitwa « *They speak with other tongues* » (Wanaongea kwa ndimi nyingine), kilichoandikwa na John Sherill. Majuma machache kabla ya ritriti yetu walihudhuria mkutano wa sala wa madhehebu mbalimbali uliojaa Roho Mtakatifu huko Pittsburgh. Pale watu waliwaombea Wakatoliki hao wanne toka Duquesne ili wamiminiwe Roho Mtakatifu. Hatukujua hayo, hata hivyo niliona kwa dhahiri miminiko hili jipya la Roho Mtakatifu katika amani na furaha ya mtu huyo alipoongea.

Baada ya mafundisho juu ya Maria, tulikuwa na ibada ya upatanisho. Katika Injili ya Mt. Yohane tunaambiwa kwamba Roho Mtakatifu anapokuja, atauthibitishia ulimwengu kuwa una dhambi. Na ingawa hiki kilikuwa kikundi kizuri sana cha vijana, tulikuwa na **hitaji kubwa sana la toba**. Kulikuwa na kununa kwingi, kulalamika kwingi, kuhukumiana kwingi, na mafarakano. Roho Mtakatifu alipokuja katika ibada ya upatanisho jioni ile alituhakikishia sote kwamba tuna dhambi. Nilisikia roho halisi ya toba inanishika.

Siku iliyofuata tuliitumia kwa kujifunza Matendo ya Mitume. Ilikuwa ya maana hasa kwamba somo juu ya sura ya pili ya Matendo ya Mitume lilifundishwa na mwanamke aliyejaa Roho Mtakatifu ambaye maprofesa wetu walimkuta juzi hivi katika kikundi cha sala. Niliposikia kwamba si Mkatoliki, lazima nikubali tu

kuwa nilikuwa na mashaka. Alianza kwa kusema: “Kwa kweli sijui nakuja kusema nini hapa. Nimesali tu na kumwomba Roho Mtakatifu aniongoze”. Hii ilinihangaisha kwelikweli. Hakuwa hata na heshima ya kutayarisha somo lake kwa ajili yetu! Ndiyvo nilivyofikiri. Lakini, mwanamke huyo mzuri alipoanza kuzungumza, Mungu alitembea kati ya watu. Mama huyo alikuwa rahisi wa kumwelewa. Kwanza nilifikiri anachosema haiwezekani. Aliongea juu ya kumjua Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi binafsi. Aliongea juu ya nguvu ya Roho Mtakatifu ambayo unaweza kuionja katika maisha yako ya kila siku. Ingawa nilianza na tabia ya kupinga, kabla hajamaliza kusema niliandika maneno hayo ili niyakumbuke: “Yesu, tafadhali, uwe halisi kwangu mimi. Uwe halisi kwangu kama ulivyo kwake mama huyo.“

Katika majadiliano yaliyofuata mazungumzo ya mama huyo, mmoja wa vijana katika kikundi changu cha majadiliano alipendekeza, kwamba mwisho wa ritriti turudie Kipaimara chetu. Kila Paska sisi Wakatoliki tunarudia ahadi zetu za Ubatizo. Yeye alipendekeza kwamba kama vijana wazima tumwalike Roho Mtakatifu aliyekuja kwetu katika Kipaimara amiminwe na kufanya nasi atakavyo. Nilimkuta kijana huyo kwa mara ya kwanza, lakini nilikubali kwamba wazo hili ni zuri kweli. Nikamwambia kwamba hata kama hakuna mwingine anayetaka kufanya hivyo, mimi nataka. Hata nikaweka juu ya ubao wa matangazo karatasi yenye maneno haya: “Ninataka mwujiza“. Nafikiri inafaa kufahamu kwamba Roho Mtakatifu alipotembea kati yetu baadaye jioni ile, alichagua kumshukia kijana huyo na halafu kinishukia

mimi kwa haraka sana. Tuliomba kumpata Roho Mtakatifu zaidi na kwa hiyo tulipokea mpako wake.

Jumamosi jioni orodha ya ritriti ilionyesha kuwa tutakuwa na tafrija kwa ajili ya kukumbuka siku ya kuzaliwa ya wanafunzi wachache. Lakini tafrija kwa kweli haikufanywa tu. Kulikuwa na aina ya ulegevu au uchovu. Watu walizungukazunguka tu. Kwa kweli tulikuwa na shida na nyumba ya ritriti. Hakukuwa na maji kwa kipindi. Mabomba fulani yalivunjika na tuliambiwa kwamba inawezekana kikundi kizima kiende nyumbani mapema. Lakini wanafunzi wachache walisukumwa kwenda katika kikanisa kidogo na kuomba ili maji yarudi kwa jina la Yesu. Baada ya sala walifungua bilula (bomba) na maji yakatoka kwa nguvu sana! Si ajabu kwamba maji yanatumika mara nyingi kama mfano wa kumweleza Roho Mtakatifu. Wengi katika Kanisa siku hizi wangesema: “Maji yamekwisha“. Lakini kwa jina la Yesu lipo tiririko jipya la maji ya uhai ya Roho Mtakatifu kati yetu!

Kwa sababu tafrija ya kusherekea siku ya kuzaliwa ya wanafunzi wale haikuanza, niliamua kwenda katika sehemu mbalimbali ya nyumba ya ritriti ili kukusanya wanafunzi wote katika chumba kimoja ili kuadhimisha sikukuu. Katika kuzunguka hivi nilifikia orofa ya pili ya nyumba ya ritriti, nikaingia katika kikanisa. Sikuingia ili nisali – bali niwaambie wanafunzi wowote washuke na kuja kwenye tafrija. Lakini nilipoingia katika uwepo wa Yesu katika Sakramenti Takatifu na kupiga magoti pale, nilijaa na hali ya kusikia uchaji sana; Siku zote niliamini, kwa kipaji cha imani, kwamba Yesu kweli yumo katika

Sakramenti Takatifu, lakini nilikuwa sijawahi kung’amua utukufu wake. Nilipopiga magoti pale, mwili wangu ulitetemeka sana mbele ya utukufu wake. Nilisikia kweli hofu na nilijiambia: “Toka hapa haraka kwa sababu kitu fulani kitatokea kwako ukiendelea kukaa katika uwepo wa Mungu“. Lakini, hamu ya kubaki mbele ya Bwana ilikuwa kubwa kuliko hofu ile.

Kijana aliyekuwa kiongozi wa wanafunzi katika ritriti aliingia katika kikanisa akapiga magoti karibu na mimi. Nikamweleza yale niliyong’amua. Alisema : “Kinatokea kitu falani, kitu ambacho hatukupanga. Wewe baki hapa na usali tu“.

Aliponiacha na mimi niko magotini mbele ya Bwana, kwa mara ya kwanza katika maisha yangu, nilisali sala ambayo ningeiita **sala ya kujitoa bila masharti**. Nilisema : « Baba, natoa maisha yangu kwako na chochote unachotaka kwangu, ndicho ninachochagua. Ikiwa ni mateso, basi nakubali. Ila tu unifundishe kumfuata Mwana wako Yesu na kujifunza kupenda jinsi yeye anavyopenda ». Wakati niliposali sala hiyo, nilikuwa napiga magoti mbele ya Bwana. Muda si muda najikuta nimesujudia, nalala usoni kabisa, nikiwa nimejinyosha mbele ya tabanakulo. Hakuna aliyenigusa. Mambo yalivyoendelea hivi viatu vyangu vikatoka katika miguu yangu. Baadaye nikatambua ya kuwa kwa kweli niko katika mahali patakatifu. Nilivyolala pale **nilifurikiwa na hali ya kufahamu huruma na upendo wa Mungu**, hasa upumbavu wa upendo wa Mungu. Hakuna chochote tunachoweza kufanywa, wala wewe wala mimi, ili kustahili upendo wa Mungu. Kamwe

haiwezekani. Mungu ni Mungu wa upendo. Ni kama maumbile yake kupenda. Sisi ni watu wake. Ni mali yake. Upendo wa Mungu unamwagika juu yetu tu, haidhuru tumefanya nini, haidhuru sisi ni nani. Maneno ya Mt. Augustino yaeleza vizuri sana niliyoona wakati huo : « Umetufanya kwa ajili yako, ee Bwana, na mioyo yetu haina raha mpaka ipumzike ndani yako ». Nilijua kwamba ikiwa naweza kung'amua upendo na huruma, upole na wema wa Mungu hivi, basi, inawezekana kwa kila mtu, ndiyo kwa kila mtu, kumg'amua Mungu pia. Ingawa nilitaka tu kukaa na kujifurahisha katika uwepo wa Bwana, nilijua kwamba nahitaji kushirikisha mang'amuzi hayo na wengine. Nilipoinuka niliwaambia wanafunzi wengine wawili waliokuwapo katika kikanisa : « Naomba haya yatukie kwenu ».

Mara moja nilimtafuta na kumpata padre aliyekuwa mchungaji pale na nilimwambia yote yaliyotukia. Aliniambia kwamba kijana aliyetaka kurudia Kipaimara chake alikuwamo katika kikanisa kama saa moja iliyopita na alikuwa na mang'amuzi karibu yaleyale. Yeye naye alianguka chini Roho Mtakatifu alipokuja juu yake. Watu wengine wanatumia maneno haya : « kulazwa katika Roho Mtakatifu ». Mimi napenda zaidi kusema : Nimeondolewa miguuni pangu kwa upendo wa Mungu .

Nilimwuliza padre nimshirikishe nani mang'amuzi haya. Maneno yake yamerudia kupata sauti katika moyo wangu kwa muda wa miaka karibu ishirini tangu siku ile. Alisema : « Bwana atakuonyesha, Bwana atakuonyesha ». Halafu nikamwuliza, Bwana amewezaje

kumtumia mtu mdogo kama mimi. Na alinikumbusha kwamba Yesu alipoingia Yerusalemu, aliketi juu ya punda. Anaweza kumtumia yeyote na chochote anachotaka tu !

Na nilipomaliza mazungumzo haya, wanafunzi wachache wa ritriti walikuja kwangu na kuuliza : « Kitu gani kilitukia kwako ? Uso waka unaonekana tofauti : » Katika barua ya pili kwa Warorintho Mt. Paulo anasema kwamba sisi sote ambao nyuso zetu hazikufunikwa, tunaonyesha kama katika kioo utukufu wa Bwana, na tunabadilishwa toka utukufu hadi utukufu, 2 Kor 3 :18. Sikutambua kwamba nilionekana tofauti, lakini kwa kadiri ilivyoonekana wasichana hawa waliona katika uso wangu kama katika kioo aliyofanya Mungu katika moyo wangu, yaani yanarudishwa kama picha katika kioo. Niliwaambia kwamba niliyang'amua yote tuliyoyazungumzia katika wikiendi hiyo. Kwa vile nilivyokuwa msichana niliyezoea kuogopa kuzungumza juu ya Yesu, nimegeuka ghafla kuwa mshujaa. Niliwachukua kwa mikono na kuwaambia : « Njooni katika kikanisa pamoja nami ». Tukapiga magoti mbele ya Bwana nikaanza kusali. Hii ilikuwa sala ya kwanza kwa ajili ya kuombea ubatizo wa Roho Mtakatifu kati ya Wakatoliki. Nilisema tu : « Bwana, chochote ulichofanya kwa ajili yangu, ukifanya kwa ajili yao ; chochote ambacho ndiyo kwanza ufanye kwa ajili yangu, ufanye kwa ajili yao ! » Hii ilikuwa semina ya maisha ya kiroho iliyokuwa fupi kuliko zote zinazokumbukwa ! Alleluya !

Ingawa hakuna aliyowaambia wale wa chini waache tafrija, haikuchukua nusu saa mpaka wanafunzi wote

wawepo katika kikanisa. Mungu aliwatembelea kwa nguvu na enzi. Tulipokuwa tumepiga magoti pale, mambo kadhaa yalitukia. Wengine walilia machozi. Baadaye walituambia kwamba walihisi upendo wa Mungu kwa ajili yao kiasi kwamba hawakuweza kufanya chochote ila kulia tu. Wengine walicheka kipumbavu. Walianza kucheka tu na wakacheka na kucheka na kucheka. Wengine kama mimi mwenyewe walisikia joto jingi katika mikono yao au linakwenda katika mikono hadi mabegani kama moto. Wengine walihisi kuna sauti kama ya kidoko katika koo lao au msisimko katika ndimi zao. Lazima ukumbuke kwamba hatukujua lolote kuhusu karama za Roho Mtakatifu. Labda tungaliweza kuongea katika lugha sote papo hapo, lakini hatukujua tujitoaje hata kupata karama hiyo. Mmoja wa maprofesa aliyekuwa amebatizwa katika Roho Mtakatifu kama mwezi mmoja uliopita, aliingia katika kikanisa na akatutazama. Alisema: “Askofu atasemaje atakaposikia kwamba vijana wote hawa wamebatizwa katika Roho Mtakatifu?” Nilisikia neno lile, kubatizwa katika Roho Mtakatifu, na nilijiuliza maana yake ni nini. Bado hatukutambua kikamilifu yaliyotukia kwetu.

Tangu mwanzo wa mambo hayo Shetani akatenda kazi yake. Jioni ile Roho Mtakatifu alipokuwa anaanguka kwa enzi na karama za Roho Mtakatifu ndivyo watu walizihisi, kijana mmoja mwanamke alisema: “Nimehisi kitu fulani kimeniingia ambacho kimenijaza kwa chuki.” Ilikuwa ni wazi kwamba ni pepo mbaya. Alijisikia anasukumizwa na pepo huyo aondoke pale na akazurura katika barabara fulani peke yake. Ilibidi fulani aende kumfuata na kumrudisha. Siku iliyofuata alikuwa katika

maumivu makali. Tulipokuwa tunafunga safari na kuondoka katika nyumba ya ritriti, nilimwona amejikunyata chini. Mmoja wa maprofesa aliyekuwa amekwisha batizwa katika Roho Mtakatifu alikuja akanipata mimi. « Njoo, Patti, lazima twende huko na kumfukuza Shetani ». Sikujua hata kama niliamani kwamba kuna pepo mbaya sembuse kuwafukuza. Lakini nilimwamini padre huyo. Aliniambia : « Uamuru kwa jina la Yesu kwamba pepo mbaya aondoke ». Nilifanya alivyoniambia na mara tu msichana akatulia. Alikuwa ametuliza kweli lakini alishangazwa. Alituambia kwamba jioni iliyotangulia wakati kila mtu alikuwa na heri na kufurahi tu, yeye alisikia chuki ya kutisha sana juu ya yote yaliyotukia. Halafu akasema kwamba ingawa alimchukia kila mmoja katika kikanisa, alinichukia mimi kuliko wote. Wakati Roho Mtakatifu alipomiminwa kwa enzi, Shetani mara alijaribu kutia wasiwasi na kuharibu kazi ya Mungu. Lakini Bwana alipata ushindi na anaendelea kupata ushindi ! Alleluya!

Tuliporudi huko Duquesne maneno ya Zaburi 126:1-3 yanaeleza vizuri mang’amuzi yetu.

> “Bwana alipowarejeza mateka wa Sayuni,
> Tulikuwa kama waotao ndoto.
> Ndipo kinywa chetu kilipojaa kicheko,
> Na ulimu wetu kelele za furaha.
> Ndipo waliposema katika mataifa,
> Bwana amewatendea mambo makuu.“

Kweli Mwenyezi Mungu alitutendea mambo makubwa, tulifurahi kwelikweli! Nilimsikia mwanafunzi mmoja wa darasa langu akisema: “Umepata kitu gani, Patti? Kama singekufahamu vizuri, ningesema, kwamba umelewa!”

Hakika nilifurahishwa kusikia hivyo, kwa sababu nilikuwa nimesoma katika Mdo 2:13, kwamba jambo lilelile lilisemwa juu ya Mitume baada ya Pentekoste.

Katika majuma yaliyofuata **polepole tulianza kugundua karama za Roho Mtakatifu** – Karama za kuponya, karama ya unabii, karama ya lugha na ufafanuzi wake. Ni majuma machache tu baada ya mang'amuzi yetu huko Duquesne tulipoambiwa kwamba wanaume wawili waliokuwa viongozi wa Cursillo watakuja kututembelea. Niliyojua juu yao ni kwamba mmoja jina lake ni Ralph na mwingine jina lake ni Steve. "Ralph na Steve" walikuwa Ralph Martin na Steve Clark! Nilikuwa na daftari la kuandika habari muhimu wakati ule uliofuata ritriti nikaandika mle yafuatayo: "Bwana, najua kwamba viongozi wawili wa Cursillo watakuja kesho, wanaoitwa Ralph na Steve. Najua kwamba Wewe ukija kwao, basi, utakuja katika Marekani ya kaskazini na katika ulimwengu wote". Sikufahamu hata majina yao ya ukoo, hata hivyo Mungu alinifunulia kwamba atawatumia watu hao wawili ili kueneza ubatizo katika Roho Mtakatifu katika mataifa, na amefanya.

Kongamano la kwanza la Notre Dame (Bikira Maria) nililohudhuria, lilikuwa Septemba 1967. Tulikuwa watu hamsini. Tuliweza kukaa wote katika chumba kimoja chenye vibao kupigiliwa ukutani. Miaka michache baadaye tu, kwenye kongamano jingine la Notre Dame, nilisimama katika uwanja wa mpira pamoja na Wakatoliki 35,000 waliokuwa wamebatizwa katika Roho Mtakatifu. Sasa tuko mamilioni toka ulimwenguni kote. Mungu tu peke yake anajua watu wangapi wamebatizwa

kwa mang'amuzi haya makubwa sana ya miminiko la Roho Mtakatifu. Yote ni kazi ya Mungu tu ! Uamsho wa kikarismatiki umeenea sana katika Kanisa Katoliki lote wakati huu, kwa sababu Mungu aliamua kutenda kazi kwa nguvu.

Pengine pengine nimeulizwa, kwa sababu nilikuwapo huko Duquesne, ninajisikiaje kwa vile nilikuwapo pale mwanzoni kabisa na nikiona yaliyotukia tangu hapo. Jibu langu ni kwamba najisikia sana nimeunganika na Maria. Najisikia sana kwamba nimekamatwa katika fumbo la Maria na jibu lake kwa Mungu. Kwa ajili yako wewe nataka kusema hivi : « Ndiyo » moja inaweza kuleta tofauti kubwa sana ! « Ndiyo » moja inayoweza kufanya ! Ni ajabu tu ! Maria alisema « Ndiyo » Roho Mtakatifu alipomjilia juu yake. Unajua yaliyotukia – yaani Yesu Kristo alizaliwa ! Na Roho Mtakatifu alipotujilia juu yetu, kila mmoja wetu alisema « Ndiyo » kwa Mungu kwa njia fulani alichukua mimba ya Yesu. Sasa **tuna utume wa kumpleka ulimwenguni**. Nikiwa sehemu ya kazi hii ya Roho Mtakatifu tangu miaka ishirini sasa, naona nimeingia katika fumbo la kazi ya Maria – yaani kukubali tendo la Roho Mtakatifu ili Yesu aweze kupelekwa ulimwenguni. Ni mang'amuzi yanayonyenyekesha sana. Na ni mang'amuzi ya uchaji sana. Kwa sababu hiyo nimeifanya Magnificat ya Maria kuwa yangu : « Mwenye nguvu amenitendea makuu na jina lake ni takatifu ». Lk 1 :49.

Ni heshima kubwa sana kwamba Bwana ameniruhusu kuwapo huko Duquesne miaka ishirini iliyopita, lakini sitaki tu kuwa sehemu ya wakati uliopita na kuyasikiliza

mambo ya zamani. Wala sitaki tu kuwa sehemu ya wakati huu. Nataka kuwa sehemu ya **wakati ujao** na ya kazi kubwa mno ambayo Mungu ataitenda ! Nimehisi sasa kwa muda wa miaka michache kwamba Bwana ataleta wimbi jipya la Roho Mtakatifu. Wale kati yetu waliokuwa sehemu ya wimbi la kwanza miaka ishirini iliyopita, basi, hajaona kitu bado ! Wimbi jipya limeanza, lakini linahitaji kuja bado. Ninaamini kwamba kila mmoja wetu anatakiwa kuwa sehemu ya wimbi jipya hili la Roho Mtakatifu, yaani ya kazi hii kubwa mno ya uinjilishaji itakayoanza kwa nguvu. Na, je, unajua kwa namna tani tunaweza kuwa sehemu yake ? Basi, umwombe Mungu ! Kwa kumwomba Mungu tu utakuwa sehemu yake!

Nilipomwomba Bwana anipe neno la pekee ili kulishirikisha na wewe, aliniongoza kusoma fungu moja katika Luka. Bila shaka unalijua sana. Nina hakika kwamba umelisikia mara nyingi. Hata hivyo, Bwana aliponiongoza kwenye neno hili, lilikuwa kama ni kweli kwa namna mpya. Nilimhisi Bwana akiniambia : “Patti, uniombe yale unayohitaji. Uniombe yale unayohitaji. Je, umewahi kuniombe kitu chochote, ambacho sikukupa? Je, umewahi kunitegemea kabisa na halafu nimekutupa tu? Uniombe yale unayohitaji“. Yesu anaongea na sisi sasa hivi katika maneno ya Luka, sura ya 11: “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe ? Au samaki, badala ya samiki atampa nyoka ? Au akimwomba yai, atampa nge ? Basi,

ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu (kibora kabisa kuliko vipaji vyote) hao wamwombao ? », Lk 11 :9-13.

Kaka na dada, tuliamini neno lake. Tumwombe zaidi na zaidi Roho wake Mtakatifu. Tunapomkaribia, tunahitaji msimamo huu : Tunakwenda kuomba kwa unyenyekevu, kwa sababu tunajua kuwa sisi ni wadogo sana. Tunakwenda kuomba kwa toba, kwa sababu tunajua kwamba tu dhaifu, wenye dhambi, tumefanya makosa. Tutakwenda kuomba kwa mategemeo makubwa sana, siyo kwa sababu ya sisi tulivyo, bali kwa sababu ya Yeye alivyo na ya yale aliyotuahidia. « Omba ! Omba ! », anatuambia. Tulitii agizo lake.

Maria yuko pamoja nasi. Alikuwapo katika chumba cha juu Pentekoste ya kwanza. Alikuwapo pamoja nasi huko Duquesne, na anaunganisha sala zake na sala zetu sasa hivi, tunapokuja mbele ya Baba. Katika Magnificat yake anatuambia: "Wenye njaa amewashibisha mema, na wenye mali amewaondoa mikono mitupu." Lk 1:53. Tukiona tunamhitaji zaidi Roho Mtakatifu, yaani aje kwa nguvu zaidi, basi, tunaweza kuwa na hakika kwamba Bwana anataka kutujaza!

**Tuombe**:
"Njoo Roho Mtakatifu! Utushukie kwa jina la Yesu; Hatujaona miujiza yako yote, ee Bwana. Hatukuona uwezo wako wote. Lakini tuliyoona, yanatufanya kupaaza sauti na kuomba zaidi. Tunataka zaidi wewe, Bwana, una mengi zaidi, na tunataka kidogo zaidi sisi,

hatuna kitu. Tunataka maisha yetu yawe katika utumishi wako, katika madaraka yako, sawa kama maisha ya Maria yaliyvokuwa. Bwana, umtume Roho wako Mtakatifu na ufanye upya uso wa ulimwengu!"

Imechukuliwa katika:

*Proclaim his marvellous deeds* (Tangaza matendo yake ya ajabu), na *How to give a personal testimony* (Namna ya kutoa ushuhuda binafsi), Patti Gallagher Mansfield. Franciscan University Press, 1987, p.41-55.